IOWA | Health and Human Services

SNAP USDA Supplemental Nutrition Assistance Program
Putting Healthy Food Within Reach

## Maswali Yanayoulizwa Sana Kuhusu Mabadiliko Mapya ya SNAP katika Jimbo la Iowa

1. **Je, ni nini kinachobadilika katika SNAP katika jimbo la Iowa?** Iowa inabadilisha bidhaa zinazoweza kununuliwa kwa kutumia SNAP katika jimbo la Iowa. Ni vyakula visivyotozwa ushuru, mbegu za mimea inayozalisha chakula na mimea inayozalisha chakula pekee vinavyotimiza masharti ya kununuliwa kwa kutumia SNAP.

2. **Je, mabadiliko haya yataanza kutumika lini?** Januari 1, 2026.

3. **Je, nitaweza kununua nini baada ya mabadiliko?** Vyakula visivyotozwa ushuru. Katika jimbo la Iowa, bidhaa hizi zinajumuisha, lakini sio tu, vitu kama vile matunda na mboga, nyama, kuku na samaki, bidhaa za maziwa, mkate na nafaka, pamoja na maziwa ya watoto wachanga.

4. **Je, sitaweza kununua nini kwa kutumia SNAP baada ya mabadiliko?** Katika jimbo la Iowa, bidhaa hizi zinajumuisha, lakini sio tu, soda na vinywaji vyenye sukari vilivyo na chini ya asilimia 50 ya juisi ya matunda au mboga, pamoja na vitu vinavyochukuliwa kuwa peremende au vilivyopakwa peremende.

5. **Je, kwa nini Iowa inafanya mabadiliko haya?** Kwa mabadiliko haya, mafao ya SNAP yataelekezwa kwenye vyakula vinavyokuza lishe bora, kama vile matunda, mboga na protini, na mbali na vyakula kama vile soda na peremende.

6. **Je, ninaweza kuomba sheria hii isitumike kwangu?** Hapana. Watu wote wa Iowa sharti wafuate sheria hii.

7. **Je, mafao yangu ya kila mwezi ya SNAP yatabadilika kutokana na mabadiliko haya?** Hapana. Mabadiliko haya hayaathiri vigezo vya sasa vya utimizaji masharti wa SNAP au kiasi cha kila mwezi cha mgao wa SNAP.

8. **Je, bado ninaweza kununua bidhaa zilizozuiliwa kwa pesa zangu?** Ndiyo.

9. **Je, bado ninaweza kutumia kadi yangu ya EBT na njia nyingine za malipo katika muamala sawa nikinunua vyakula vipya vilivyowekewa vikwazo?** Ndiyo, bado unaweza kununua bidhaa zozote zinazotozwa ushuru kwa kutumia pesa zisizo za SNAP wakati wa muamala.

Tembelea https://hhs.iowa.gov/assistance-programs/food-assistance/snap kwa maelezo zaidi.

10. **Je, hii inatumika kwa washiriki wa SNAP wa Iowa pekee?** Hapana. Sheria hii inatumika kwa mtu yeyote anayenunua chakula katika jimbo la Iowa kwa kutumia mafao ya SNAP, bila kujali ni jimbo gani limeidhinisha mafao yake ya SNAP.

11. **Je, wauzaji wote wa reja reja wanahitajika kufanya mabadiliko haya kwenye vyakula vinavyotimiza masharti ya SNAP?** Ndiyo. Maduka yote ya Iowa ambayo yanakubali SNAP yanahitajika kufanya mabadiliko haya.